**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Simu: 028-2227148
Nukushi: 028-2227140

Barua pepe: ded@karagwedc.go.tz
Tovuti: www.karagwedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya,
01 Barabara ya Ikulu,
S.L.P 20,
**35482 KARAGWE**

Kumb. Na. KGR/HWK/T.4/7D/10

18/05/2023

**YAH: TANGAZO LA KUITWA KAZINI**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

1 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilitangaza nafasi za kazi kupitia tangazo lenye **Kumb. Na**. KGR/HWK/T.4/7D/10 la tarehe **17/4/2023** kwa kada nne yaani; Mtendaji wa Kijiji daraja la III nafasi **19,** Dereva daraja la II nafasi **2**, Msaidizi wa kumbukumbu daraja la II nafasi **2**, na Mwandishi Mwendesha Ofisi daraja II nafasi **4**. Hii ilitokana na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kupata kibali cha ajira chenye **Kumb. Na. FA.97/228/01 "TEMP"/06** cha tarehe 06 Aprili, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mpya na kibali mbadala cha tarehe 31/1/2023 chenye kumb.Na.FA.170/368/01"C"/45 cha nafasi **1** ya mtendaji wa kijiji daraja la III.

2 Aidha nimepokea Maelekezo kutoka kwa Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kupitia barua yenye **Kumb. Na AB.161/259/01/D/12** ya tarehe **20 Aprili, 2023** kuwa kwa mujibu wa kanuni Na **22 (1,2)** ya kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya Ajira inaainisha kutumia kanzidata ya watahiniwa waliofaulu usaili na hawakupata kazi kwa sababu ya uchache wa nafasi.

3 Kwakuwa nilitangaza nafasi za **Mtendaji wa Kijiji daraja la III** nafasi **10**, na kufanya usaili mwezi Julai 2022 ambapo wasailiwa wengi walipata alama kubwa na kujipatia sifa za kupata kazi lakini kwa sababu ya uchache wa nafasi hawakupata nafasi na hadi sasa



Scanned with CamScanner

hawajapata kazi.Wasailiwa hao ambao ni 19 wanatakiwa kuripoti kazini ndani ya siku 07 kuanzia tarehe ya tangazo hii ili kujaza nafasi hizo . Aidha nafasi 02 za watendaji wa vijiji daraja la III zilizobaki baada ya kuchukua waliopo kwenye kanzidata na kwakuwa hakuna usaili uliokuwa umefanyika ndani yam waka mmoja za Dereva daraja la II nafasi 2, Msaidizi wa kumbukumbu daraja la II nafasi **2**, na Mwandishi Mwendesha Ofisi daraja II nafasi **4**, nafasi hizo zitafanyiwa usaili kwa waombaji waliokidhi vigezo na tarehe ya usaili itatangazwa hapo baadae.

4.Waombaji walioitwa kazini wanatakiwa kufika na:-

(a) Kitambulisho cha Uraia (National Identification Card) au namba (National Identification Number) kwa ambao hawajapata vitambulisho kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).

(b) Vyeti halisi vya kidato cha nne/kidato cha sita na cheti cha Taaluma.

(c) Cheti cha kuzaliwa.

**5. Orodha ya walioitwa kazini imeambatishwa katika tangazo hili**

6. Naomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

ADV.WILSON S. NYAMUNDA

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE



Scanned with CamScanner

**ORODHA YA WALIOITWA KAZINI NAFASI YA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III**

| NA. | JINA LA MWOMBAJI | ANWANI YA MWOMBAJI |
|---|---|---|
| 1 | SHAHIDU BURHANI | P.O.BOX 72 KYERWA |
| 2 | ATHANAS A. MAPOMBE | P.O.BOX 44 KIGOMA |
| 3 | ANUSIATHA ALBERY KADUI | P.O.BOX35 BIHARAMULO |
| 4 | STADIUS THEODORY | P.O.BOX 49 MULEBA |
| 5 | HASSAN ABDUNURU | P.O.BOX 158 BUKOBA |
| 6 | FESTACE J. KASHAIJA | P.O.BOX 203 KARAGWE |
| 7 | LINUS TINDAMANYILE | P.O.BOX 20 KARAGWE |
| 8 | DONATUS LAURIAN LEOPORD | P.O.BOX 72 KYERWA |
| 9 | DELIVA DENIS MSHOMESA | P.O.BOX 72 KYERWA |
| 10 | OCTAVIUS OSWARD KAKURU | P.O.BOX 196 KARAGWE |
| 11 | JACKSON L. DAUSON | P.O.BOX 491 BUKOBA |
| 12 | HAPPYNESS PAUL | P.O.BOX 329 TABORA |
| 13 | SADELIN M. SOSPETERY | P.O.BOX 20 KARAGWE |
| 14 | ELIVIRA OSWARD WILBERD | P.O.BOX 20 KARAGWE |
| 15 | LIVASON BONIPHACE AMOS | P.O.BOX 02 KARAGWE |
| 16 | DATIVA DOMINICK | P.O.BOX376 MULEBA |
| 17 | JOANITHA K.JOHANSEN | P.O.BOX 20 KARAGWE |
| 18 | LOYCE JOHNBOSCO KAGENGERE | P.O.BOX 42 KARAGWE |
| 19 | AULEA RWOMWADI | P.O.BOX 131 MLEBA |

Scanned with CamScanner